Warithi Wa Mungu

na

Ellis P. Forsman

Warithi Wa Mungu

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 12, 2011

Warithi Wa Mungu

Rum. 8:14-18

Rum. 8:14-18, "*Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndiyo wana wa Mungu. Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa, ambayo kwa hiyo twalia, Aba yaani Baba. Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu; na kama tu watoto basi tu warithi, warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naama tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye.k kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu.*"

Tunapaswa kushukuru kiasi gani kwamba tu wana wa Mungu. 1 Yohana 3:1, "*Tazameni ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu; na ndivyo tulivyo. Kwa sababu hii ulimwengu haututambui, kwa kuwa haukumtambua yeye."*

Kuna baraka kubwa kwa mtu yule anayemchukua motto yatima, kumwasili, na kumpa makazi. Mungu ametupa upendo huu wa thamani kwa kutuasili katika familia yake, na kuturuhusu kumuita Baba yetu wa mbinguni.

Kwa sababu ya uhusiano wetu na Baba, tunachukuliwa kuwa wakuu kuliko hata Yohana mbatizaji. Mat. 11:11, "*Amini nawaambia hajatokea mtu katika wazao wa wanawake aliyemkuu kuliko Yohana mbatizaji; walakini aliyemdogo katika ufalme wa mbinguni ni mdogo kuliko yeye.*"

Ni masharti yapi ya kufanyika wana wa Mungu?

Siyo ubabu

Watu wengine hupenda kujivunia ubabu wao.

Mmoja wa watu hao kwa majivuno alimwambia Will Rodgers kwamba mababu zake walikuja wakatika wa maono. Lakini Will Rodgers akamwambia, "Babu zangu walikutana na maono."

Wayahudi wengi kindi cha Yesu walifungwa akili zao katika kujisifia mababu zao.

- Mat. 3:9, "*Wala msiwaze mioyoni mwenu kwamba tunaye baba ndiye Ibrahimu; kwa maana nawaambia ya kwamba Mungu aweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.*"
- Yoh. 8:32-33, "*Tena mtaifaamu kweli nayo hiyo kweli itawaweka huru. Sisi tu uzao wake Ibrahimu, wala hatujawa watumwa wake mtu wakati wo wote; nawe wasemaje mtawekwa huru?*"

Walidhani kwamba wanaruhusa ya kuingia katika utukufu kwa sababu walikuwa uzao wa Ibrahimu.

Siyo hekima

Wanaoitwa watu wenye hekima leo wanadhani kwamba ni upumbavu kumwegemea Mungu.

- Mit. 3:5, "*Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe.*"
- Yer. 9:23, "*BWANA asema hivi mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake.*"
- 1 Kor. 1:25-31, "*Kwa sababu upumbavu wa Mungu unahekima zaidi ya wanadamu, na udhalimu wa Mungu una nguvu zaidi ya wanadamu. Maana ndugu zangu angalieni mwito wenu, ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo, walioitwa; bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima, tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu; tena Mungu alivichagua vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa, naam, vitu ambavyo haviko ili avibatilishe vile vilivyoko. Mwenye mwili awaye yote asije akajisifu mbele za Mungu. Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi; kusudi kama ilivyoandikwa, yeye aonaye fahari na aone fahari juu ya Bwana.*"

Pamoja na kusoma kwetu kote, sisi ni viumbe vidogo mbele za Mungu.

Ulimwengu umewasiki wakina Thomas Edison na Henry Ford, lakini pamoja na ujuzi wote waliotuletea, bado hakuna walichotupa ambacho twaweza kulinganisha ushirika na Mungu.

Siyo kwa sababu unaweza kusali sala ndefu na kutoa changizo ya pesa nyingi

- Mat. 23:14-19, "*Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki, kwa kuwa mnakula nyumba za wajane na kwa unafiki, mnasali sala ndefu, kwa hiyo mtapata hukumu iliyo kubwa zaidi. Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki, kwa kuwa mnazunguka katika bahari na nchi kavu ili kumfanya mtu mmoja kuwa mwongofu; na akiisha kufanyika mnamfanya kuwa mwana wa jehanamu mara mbili zaidi kuliko ninyi wenyewe. Ole wenu viongozi vipofu, ninyi*

msemao mtu atakayeapa kwa hekalu, si kitu; bali mtu atakayeapa kwa dhahabu na hekalu amejifunga. Wapumbavu ninyi na vipofu, maana ni ipi iliyo kubwa, ile dhahabu au lile hekalu liitakasalo dhahabu?Tena mtu atakayeapa kwa madhabahu si kitu bali mtu atakayeapa kwa sadaka iliyo juu yake amejifunga. Vipofu ninyi maana ni ipi iliyo kubwa, ile sadaka au ile madhabahu iitakasayo sadaka?

- Mat. 23:23-27, "*Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani adili na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya wala yale mengine msiyaache. Viongozi vipofu wenye kuchuja mbu na kumeza ngamia. Ole wenu waandishi na mafarisayo wanafiki, kwa kuwa mnasafisha nje ya kikombe na chano, na ndani yake vimejaa unyang'anyi na kutokuwa na kiasi. Ewe Farisayo kipofu, safisha kwanza nje ya kombe ili ndani yake nayo ipate kuwa safi. Ole wenu waandishi na mafarisayo wanafiki, kwa kuwa mmefanana na makaburi yaliyopakwa chokaa, nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa mifupa ya wafu, na uchafu wote.*"

Mtu anaweza kufanyika mwana wa Mungu tu kwa "*kuzaliwa mara ya pili*"

Yoh. 3:3-5, "*Yesu akajibu akamwambia, Amin, Amin, nakuambia mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu. Nikodemo akamwambia awezaje kuzaliwa mtu akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? Yesu akajibu akamwambia, Amin, Amin, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.*"

Mfumo huu pia unazungumziwa katika Agano Jipya kama "kuongoka." Mat. 18:3, "*Akasema Amin nawaambia msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.*"

Pia ni kufanya mapenzi ya <u>Mungu</u>. Mat. 7:21, "*Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye wa mbinguni.*"

Ni kuwa kiumbe kipya.

- Gal. 3:27, "*Maana nyinyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*"

- 2 Kor. 5:17, "*Hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, tazama yamekuwa mapya.*"

- Rum. 6:3-4, "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba , vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*"

Kwa kuwa wana wa Mungu, tunafanywa kuwa warithi wake

Rum. 8:17, "*Na kama tu watoto, basi tu warithi; warithi wa Mungu warithio pamoja na Kristo; naam tukiteswa pamoja ili tupate na kutukuzwa pamoja naye.*"

"*Na kama tu watoto basi tu warithi*"

Hiyo ni, kama tukizaliwa mara ya pili tunaingizwa katika familia ya Mungu, na kufanywa warithi; hivyo basi tutahudumiwa kama wana wa kiume na kike na tutapewa kipaumbele cha kushiriki huruma ya familia ya Mungu.

"*Warithi wa Mungu*"

Hivyo, sisi sote tutakuwa washiriki wa urithi huo ambayo Mungu anatoa kwa wanawe.

Kama wana wa Mungu, tunapokea huruma zake na baraka hapa na sasa; lakini urithi unatusubiria katika umilele baada ya maisha haya tutakapohamia katika mji mpya ambao unaandaliwa kwa ajili yetu.

Hii ni heshima kuu ya juu kuliko kuwa mrithi wa unalikia wa dunia hii, au kuwa wana wa kiume na kike wa ufalme wa juu wa dunia hii.

"*Warithio pamoja na Kristo*"

Hiyo ni, warithi wenza pamoja naye – kushiriki pamoja na Kristo.

Yesu ni Mwana wa Mungu, na kwa hivyo ni mrithi katika heshima yote na utukufu wa mbingu.

Lakini Wakristo wanaungana pamoja naye; wao ni ndugu zake; alafu pia bado ni washiriki wa utukufu wake na heshima.

Tu wana wa Mungu katika mitazamo tofauti Yesu alivyo. Ni Mwana wa Mungu na uhusiano wa hali ya juu; lakini tu wana wa Mungu kwa uasili, alafu bado wazo la kuwa wana bado liko pale pale.

"*ikiwa ndivyo ba twateswa pamoja naye*"

Kama tukiteswa kwa ajili yake na kubeba mateso kwa ajili yake, hivyo tunaonyesha kwamba tumeungana pamoja naye.

Hatuteseki kama Yesu alivyoteswa, lakini tunaweza kushirki katika roho yule yule ambapo alibeba mateso yake kwa ajili yetu.

- Mdo. 14:22, "*Wakifanya imara roho za wanafunzi na kuwaonya wakae katika ile Imani nay a kwamba imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi.*"
- 1 Pet. 4:13, "*Lakini kama mnavyoshiriki mateso ya Kristo, furahini ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe.*"

"*ili tuweze kutukuzwa pamoja*"

Kama tukiungana pamoja naye katika mfumo huo wa mateso, tunatarajia pia kuungana pamoja naye katika mfumo huo wa hitimisho – zaidi ya mateso yote na majaribu.

- Fil. 3:10, "*Ili nimjue yeye na uweza wa utukufu kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake.*"
- 2 Tim. 2:11-12, "*Ni neno la kuaminiwa kwa maana , kama tukifa pamoja naye, tutaishi pamoja naye pia, kama tukistahimili tutamiliki pamoja naye; kama tukimkana yeye naye atatukana sisi.*"
- 2 Tim. 3:12, "*Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa.*"

Baadhi ya vitu ambazo sisi ni warithi wayo

Warithi wa neema yake (upendeleo)

- Rum. 5:1-2, "*Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokanayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo mnasimama ndani yake, na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu.*"
- Rum. 10:17, "*Basi imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.*"
- Tit. 2:11-12, "*Maana <u>neema</u> ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo <u>yatufundisha</u> kukataa ubaya na tama za kidunia, tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa katika ulimwengu huu wa sasa.*"

Mpango wake wa wokovu ni zawadi yake ya upendeleo kwa wanawe

Kama tunamfahamu mtu tajiri tungeweza kusikia akituambia, "Ninyi ni rafiki zangu; kama nikiwasaidia kwa njia yo yote, basi mnifahamishe."

Tayari tunarafiki ambaye anaweza kutupa upendeleo mkuu. Upendeleo wa Mungu uliopo unapaswa umanishe mengi zaidi kuliko cho chote katika ulimwengu huu.

Ebr. 4:14-16, "*Basi ikiwa tuna kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, yesu Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu. Kwa kuwa hakuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa katika mambo yote sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.*"

Warithi wa wokovu

Ebr. 1:14, "*Je! Hao wote sir oho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu.*"

Wokovu kupitia Kristo ni silaha katika mpango wa Mungu wa ukombozi.

- Efe. 1:10, "*Yaani kuleta madaraka ya wakati mkamilifu, atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia. Naam, katika yeye huyo;*"
- 2 Tim. 2:10, "*Kwa ajili ya hilo nastahimili mambo yote, kwa ajili ya wateule ili wao nao waupate wokovu ule ulio katika Kristo Yesu, pamoja na utukufu wa milele.*"
- Tit. 2:11, "*Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa.*"

Warithi wa ahadi zake

- Gal. 3:29, "*Na kama ninyi ni wa Kristo basi mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi.*"
- Ebr. 6:17, "*Katika neno hilo Mungu akitaka kuwaonyesha zaidi sana warithio ile ahadi, jinsi mashauri yake yasivyoweza kubadilika, alitia kiapo katikati.*"

Wanadamu wakati mwingine uweka ahadi ambazo hawawezi kutimiza, lakini Mungu hayuko ivyo. 2 Pet. 3:9, "*Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali*

huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba."

Warithi wa ufalme

- Yak. 2:5, "*Ndugu zangu wapenzi sikilizeni, Je! Mungu hakuwachagua maskini wa dunia wawe matajiri wa imani na warithi wa ufalme aliowahidia wampendao?*"
- Yoh. 14:15, "*Mkinipenda mtazishika amri zangu.*"

Watu wengi walio katika nchi ambazo zimekumbwa na majanga walilazimika kuhama ili kuokoa maisha yao, na urithi wao katika serikali yao wameukataa, lakini sisi ni warithi wa ufalme wa Mungu katika hali halisi.

Tunauthamani wa uzima ambao Kristo ameeleza katika kumiliki ufalme na akatumilikisha. Mat. 5:3, "*Heri walio maskini wa roho; maana ufalme wa mbinguni ni wao.*"

Warithi wa uzima wa milele

- Tit. 3:7, "*Ili tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu.*"
- 1 Pet. 1:4-5, "*Tupate na urithi usioharibika usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu. Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho.*"
- 1 Pet. 1:9, "*Katika kuupokea mwisho wa imani yenu, wokovu wa roho zenu.*"
- 1 Yoh. 2:25, "*Na hii ndiyo ahadi aliyotuahidia, yaani uzima wa milele.*"

Kwa nini majina ya wafu huwekwa katika mawe yalioko makaburini? Ili kwamba majina yao ya endelee kukaa; ili kwamba tuweze kuyakumbuka.

Wanadamu wakati Fulani huacha majina yao, au majina yao yanaweza kuwekwa katika mawe ya msingi ya kwenye jingo. Ambacho kinapaswa kuwa muhimu kwetu ni kwamba majina yetu yameandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana Kondoo?

- Luka 10:20, "*…furahini kwa maana majina yenu yameandikwa mbinguni.*"

- Fil. 4:3, "*Na kujitahidi kuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani.*"
- Ebr. 12:23, "*Mkutano mkuu wa kanisa la mzaliwa wa kwanza, walioandikwa mbinguni na Mungu mwamuzi wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika,*"

Hivyo tukiwa wana wa Mungu waliokamilika, majina yetu yataishi na kuishi; na miili yetu ikioza kwa sababu ya kifo, nafsi zetu zitaishi milele katika jamii iliyobarikiwa ya walio okolewa.

Warithi wa vitu vyote

Ufu. 21:7, "*Yeye ashindaye atarithi vitu vyote; nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu.*" Hapa Yohana anahitisha mambo yote.

Hebu fikiria kama ungekuwa mrithi wa kiti katika nchi kubwa. Lakini, kama wana wa Mungu, ni warithi wa kila kitu katika ufalme wa Mungu; ninyi ni warithi wa "*vitu vyote*" vya milele.

Hitimisho

Je inamanisha kitu kwako kuwa mwana wa Mungu?

Je inakufanya ufurahi na kushangilia kwa uhusiano huo ulioinuliwa?

Kwa nini tuna nung'unika katika huduma yake? Kuna baadhi ya watoto wake wanaofanya kazi ndogo sana, na kuwa kana kwamba wana shinikizwa.

Wale wanaofanya kazi ndogo wanajikuta wenyewe wakiingia katika matatizo.

Nilipokuwa motto tukiishi katika shamba, kuna kazi zingine ambazo nilitakiwa kuzifanya (kukamua, kulisha kuku, kulima, kufanya kazi katika karakana, etc). Watoto wa jirani wakadhani kwamba wazazi wangu walikuwa wananionea. Hawakuwa na majukumu makubwa na walikuwa wakijikuta katika matatizo makubwa katika jamii, wakifanya vitu ambazo hawapaswi kufanya.

Kuwa wana wa Mungu, hakuna kazi kubwa kwetu. Tunapaswa kuangalia majukumu yetu; tukikubali changamoto na majaribu mbele yetu.

- Rum. 8:31, "*Basi tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwa upande wetu ni nani aliye juu yetu?*"

- 2 Kor. 9:8, "*Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi ili ninyi mkiwa na riziki za kila namna siku zote mpate kuzidi sana katika kila tendo jema.*"

- Fil. 4:13, "*Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.*"

Wale ambao si wana wa Mungu wanakataa wenyewe furaha na amani ya maisha ya ukristo, pamoja na baraka zinazowasubiri wana wa Mungu katika umilele.

Kama una utajiri wote na umaarufu wa dunia, na siyo mwana wa Mungu, umepotea.

Lakini Mungu hawezi kukutumia hadi unyenyekee katika mapenzi yake. Tunawezaje kufanywa warithi wake? Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani**. Ebr. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*" Nilipokuwa katika shule ya sekondari (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na wa kwangu akaniambia kwamba alikuwa hamwamini Mungu, kwa vile nilikuwa nimebatizwa nilichukua nafasi kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaona kuwa kuishi maisha ya Ukrsto ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kama Mungu yupo. Lakini ili awe sehemu salama labda anapaswa kwenda kanisani, na siku akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kwamba alihudhuria kanisani na kuishi maisha mema kwamba Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na sio motoni (kama kuna moto). Nikamwambia "hayaendi hivyo. Unapaswa umwamini kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza."

- **Toba**. Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Mdo. 11:18, "*…Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao <u>toba liletalo uzima</u>.*" Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba nyingine, na unafikiria mwenyewe, "kuna mwizi ndani ya nyumba hii!" hivyo unachukua simu ya mkononi, taratibu unawapigia polisi, ukiwaambia kwamba kuna mwizi ndani kwako, na unawapa anwani yako. Muda kidogo unawasikia polisi wamefika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, "Samahani, Samahani!" anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu

amekamatwa; na sio kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataibatena na kwamba anataka kubadili maisha yake ili kwamba asiibe tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloongoza katika badiliko la tendo. tunapaswa kufanya hivyo kabla hatujafanyika Wakristo.

- **Kiri.** Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka. Maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

  Kumbuka andiko hilo hapo juu kwamba (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekea katika kutu fulani; sio kwamba mtu tayari ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ambapo haki, uzima, na wokovu hupatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikasema, huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninaye pendezwa naye.*" (Mat. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema kwamba ni kitu sahihi kufanya. Unaona jinsi Mungu alivyopendezwa wakati Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Ndivyo **itupasavyo** kuitimiza haki yote.*" Tunabatizwa kwa sababu inatiza haki yake, na sio kwa sababu ya haki yetu.

  Hakika, tusipobatizwa, bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Mdo. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu".* Kwa nini mtu aache atua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

  Yesu aliagiza kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*"

  Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Basi sasa unakawilia nini? Simama ubatizwe ukaoshwe*

dhambi zako, ukiliitia jina lake." (Mdo. 22:16). Ubatizo ni hitaji ambalo Mungu ametupatia.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Rum. 6:4). Utu wetu wa kale lazima ufe. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, viyvo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama tulivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika tutaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; tukijua neno hili ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike tusitumikie dhambi tena;*" (Rum. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumika katika damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tuko huru na dhambi zetu za kale pale tu tunapo batizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatupeleki mwili makaburini na kuuwekea udongo kidogo juu yake; bali tunauzika.

Kama haujafanyika Mkristo, kwa nini usifanyike leo.